Toleo 75 - Ramadhan 1444 H / Aprili 2023 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Ushoga ni Agenda ya Wamagharibi, Matunda ya Mfumo Wake wa Kidemokrasia

**HABARI NA MAONI**
Tafuteni Kheri kutoka kwa Wanajeshi wa Waislamu

**MATOLEO**
Athari za Ushawishi wa Kijamii juu ya Waislamu Leo

**JIBU LA SWALI**
Zaka juu ya Bidhaa za Biashara



# Pongezi kutoka kwa Amiri wa Hizb ut Tahrir, Mwanachuoni Mkubwa, Ata bin Khalil Abu Al-Rashtah, kwa Wanaozuru Kurasa zake kwa Mnasaba wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan wa Mwaka 1444 H Sawia na 2023 M

Kwa Umma bora ulioletwa kwa ajili ya wanadamu... Umma wa Kiislamu ambao Mwenyezi Mungu ameutukuza kwa utiifu Wake...

Kwa wabebaji Da’wah ambao biashara wala uuzaji haviwashughulishi na kumkumbuka Mwenyezi Mungu...

Kwa waheshimiwa wanaozuru ukurasa wanaokuja kwa ajili ya kheri unayo beba ...

Assalamu Alaikum wa Rahmatullah wa Barakatahu,

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, na rehma na amani zimshukie Mtume wa Mwenyezi Mungu, na jamaa zake, na maswahaba zake, na wanaomfuata.

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنْزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ وَمَنْ كَانَ مَرِيضاً أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِنْ أَيَّامٍ أُخَرَ يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَى مَا هَدَاكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

**“Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi. Basi ataye kuwa mjini katika mwezi huu naafunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu katika siku nyengine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na mtimize hiyo hisabu, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongoeni ili mpate kushukuru.”** [Al-Baqara 2:185]. Na Mtume (saw) amesema, kwa mujibu wa yale aliyopokewa na Al-Bukhari kutoka kwa Abu Salamah kutoka kwa Abu Huraira:

مَنْ صَامَ رَمَضَانَ إِيمَاناً وَاحْتِسَاباً غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ

**“Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhan kwa imani ya kweli, na kutaraji kupata thawabu za Mwenyezi Mungu, basi husamehewa madhambi yake yote yaliyopita.”** Ni mwezi waʹibaadah na maghfirah, na hoja za uongofu na upambanuzi (Furqan).

Kadhalika ni mwezi wa jihad na ufunguzi wa wazi ambayo ndani yake kuna Badr kubwa, na ndani yake ni kufunguliwa kwa Makka, ufunguzi mkubwa kabisa ambao ulikuwa ndio nukta kianzio kwa majeshi ya Waislamu walipobeba liwa (bendera) ya kheri hadi pembe zote za dunia... Na tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) kwamba mwezi huu mtukufu uwe mwanzo wa kheri na baraka juu ya Waislamu, ili Khilafah Rashida irudi kwa mara nyengine, nayo ni ahadi ya Mwenyezi Mungu (swt).

وَعَدَ اللهُ الَّذِينَ آمَنُوا

**“Mwenyezi Mungu amewaahidi walio muamini”** [Al-Ma’iadah 5:9] na bishara njema ya Mtume wake (saw), hapo Uislamu na Waislamu watapata izza na ukafiri na makafiri watadhalilishwa.

وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللهِ

**“Na siku hiyo Waumini watafurahi * Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu”** [Ar-Rum 30:4-5].

Wassalamu Alaikum wa Rahmatullah wa Barakatahu

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
**1 Ramadhan 1444 H sawia na 23/03/2023 M**



Pepe: info@uqab.or.ke

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 04/1444 Jumatatu, 21 Shaaban 1444 H 13/03/2023 M


**<u>Taarifa kwa Vyombo Vya Habari</u>**

# Ushoga ni Agenda ya Wamagharibi, Matunda ya Mfumo Wake wa Kidemokrasia

Kufuatia kampeni inayo endelea dhidi ya ushoga na mapenzi ya jinsia moja nchini Tanzania inayofanywa katika mikoa mbalimbali na Waislamu ikiwemo Hizb ut Tahrir Tanzania, tungependa kubainisha yafuatayo:

Kwanza, ni mfumo wa kidemokrasia ambao hutumika kama farasi kupitia dhana za 'uhuru wa kibinafsi' unaohubiri na kutetea ajenda ya Wasagaji, Mashoga, Wapenda jinsia mbili, Wanaobadili jinsia na Wanaochanganya jinsia (LGBTQ) na kila aina ya uovu, mfumo ambao ni hatari na tishio kwa ustawi wa ubinadamu, na kimsingi ni aina mpya ya dini ambayo inalazimishwa juu yetu kuacha nguvu zote za kidini, ili kuleta aina mpya ya uharibifu wa maadili. Hiyo ni dalili ya wazi inayoonesha kutofaa kwa mfumo wa kidemokrasia katika kuwahudumia wanadamu.

Kwa wafuasi wa demokrasia, wanaharakati na watetezi wa haki za binadamu, badala ya kupokea na kuhubiri kila kitu kwa upofu, ni muhimu kuelewa kwamba mfumo wa kidemokrasia wa kisekula unaohubiri 'uhuru wa kibinafsi' haukuibuka kwa msingi wa hoja, lakini uliibuka juu msingi wa kupatiliza kijanja na kwa mtazamo wa kijuha baada ya mapambano makali baina ya wanamageuzi dhidi ya makasisi juu ya nafasi ya dini katika maisha. Kilichotokea ni kuja na suluhisho la muwafaka ya kati na kati (kuridhisha pande zote mbili) ambapo kila upande ulipata kitu, kwamba watu wa dini (makasisi) watabakia na dini yao katika maeneo ya ibada, ilhali wanamageuzi watakuwa ndio wenye haki ya maamuzi nje ya mahali pa ibada, kwa mujibu wa matakwa ya demokrasia.

Pili, vitendo vya ushoga vinakuzwa na mataifa ya Magharibi kwa kutegemea Tamko la Kimataifa la Haki za Kibinadamu. Kusema kwamba vifungu vya Haki za Binadamu ni kwa watu wote (universal) ni uwongo wa wazi. Mwenye haki pekee ya kutangaza jambo kwamba ni kwa watu wote ni Muumba wa ulimwengu na wanadamu pekee, na hakuna hata mmoja katika waliotayarisha tamko hilo amewahi kudai ubora huo, badala yake wale walioandika tamko hilo wamepita zamani (walikufa). Hiyo ni dalili ya wazi kwamba tamko hilo sio kwa watu wote (kiulimwengu), kwa sababu liliandikwa na wachache miongoni mwa viumbe na sio yule aliyeumba ulimwengu.

Tatu, ajenda ya LGBTQ inaonyesha kwa uwazi hali duni ya jinsi nchi zinazoendelea zilivyo, kukosa mamlaka halisi ya kujitawala licha ya kuwa na 'uhuru wa bendera'. Maamuzi yote yawe ya kisiasa, kiuchumi, na hata kijamii kama ilivyo katika suala hili, ni kwa mujibu wa matakwa ya mamlaka ya wakoloni wa kibepari ambao hupuuza ubinadamu au maadili.

Nne, kampeni za kuunga mkono ushoga zinamdhalilisha na kumdhuru binadamu na ustawi wake, kwa kuwa kwa mchakato huu binadamu anatumiwa kama kifaa cha majaribio. Hapo awali, vitendo vya ushoga vilikuwa havikukubalika hata ndani ya nchi za kibepari za Ulaya, lakini baada ya kampeni kubwa sasa ni jambo linalokubalika. Asili ya mwanadamu hakuumbwa kama kifaa cha majaribio. Hali ya kufanya majaribio katika asili ya binadamu ni dalili ya wazi ya kutofaa hizi zinazoitwa haki za binadamu, kwa kuwa asili ya mwanadamu haiwezi kubadilika. Jambo hili lina madhara na matokeo mabaya kwa ubinadamu.

Uislamu unamtazama mwanadamu kuwa kiumbe bora kilichotukuzwa kuliko viumbe vingine vyote, ambapo asili yake ya kimsingi haibadiliki, na kamwe si kifaa cha majaribio. Mwanadamu huyu kwa kuwa ni kiumbe ana udhaifu, ikiwa ni pamoja na mipaka ya ujuzi wake, kutetea maslahi yake binafsi na kuathiriwa na mazingira. Udhaifu huu unamnyima binadamu uwezo wa kutunga sheria (kwa usahihi). Ni Muumba pekee kwa Rehema zake ndiye ana uwezo wa kulibeba jukumu la kutunga sheria (kwa usahihi) za kumuongoza mwanadamu katika kila nyanja ya maisha yake.

(يُرِيدُ اللَّهُ أَن يُخَفِّفَ عَنكُمْ وَخُلِقَ الْإِنسَانُ ضَعِيفًا)

**"Mwenyezi Mungu anataka kukupunguzieni taabu, kwa kuwa mwanaadamu ameumbwa dhaifu"** [4:28]


**Masoud Msellem**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Tanzania**

# HABARI NA MAONI
# Amiri wa Hizb ut Tahrir Tafuteni Kheri kutoka kwa Wanajeshi wa Waislamu

**Habari:**

Mazingira ya kumbukumbu ya miaka 102 ya jinai ya kuivunja Dola ya Khilafah ambayo ilifanywa na mkoloni Kafiri Magharibi kwa usaidizi wa wasaliti wa Kiarabu na Kituruki, yangali yananing'inia juu yetu mnamo tarehe 28 Rajab mwaka wa 1342 H sawia na tarehe tatu Machi mwaka wa 1924 M.

**Maoni:**

Kwa mnasaba wa kumbukumbu ya miaka 102 ya kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah, Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir iliandaa kampeni ya mtandaoni yenye kichwa: "Khilafah inasimamishwa vipi", iliyojumuisha amali mbalimbali. Kampeni yake ilifikia kilele jioni ya Jumamosi, 27 Rajab Al-Muharram 1444 H sawia na 18 Februari 2023 M, kwa kongamano maalum la kuhitimisha lililofunguliwa na Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah, Mwenyezi Mungu amuhifadhi, kwa hotuba iliyoanza kwa kuukumbusha Ummah juu ya kuvunjwa kwa Khilafah yake mikononi mwa Magharibi kafiri, ikiongozwa na Uingereza, na kwa ushirikiano wa wasaliti wa Kiarabu na Kituruki. Na jinsi historia yake ilivyokuwa giza baada ya hapo, kwani Khilafah ilikuwa dola yake ya haki na uadilifu, dola zake sasa ni zaidi ya hamsini zilizovunjika vunjika, na jeuri ya watawala wake baina yao ni kali, hata tetemeko la ardhi la Syria na Uturuki, licha ya ukali wake, halikuweza kuondoa mgawanyiko wao na kuregesha umoja wao ndani ya dola moja, na jinsi Ummah na ardhi zake zilivyoporwa na kila mwenye tamaa, hata Mayahudi wa upeo usio wa kawaida walisubutu kuushambulia, ambapo waliumiliki na kunyakua ardhi yake iliyobarikiwa.

Kisha yeye, Mwenyezi Mungu amhifadhi, akawakumbusha Waislamu kwamba uchokozi dhidi yao haukabiliwi kwa maneno ya kuvutia na yasiyo na manufaa, bali uchokozi huzuiliwa kwa makali ya upanga, kwa mapigo yanayomfanya adui asahau minong'ono ya Shetani. Hivi ndivyo walivyokuwa Waislamu walipokuwa na Khilafah, na alisambaza taswira na matukio kadhaa kutoka kwenye historia angavu ya Khilafah ambayo ni dalili ya hili.

Kisha akamalizia hotuba yake, akiielekeza hotuba yake kwa watu wenye nguvu na uthabiti katika Ummah wetu kwa kusema: "Kwa kumalizia, narudia kuwasihi enyi watu wenye uwezo na ulinzi... Nyinyi pekee ndio mnaoweza kuuponya moyo wa Ummah kutoka kwa maadui zake, maadui wa Dini yenu. Nyinyi pekee ndio mnaoweza kukomesha udhalilifu uliowafikia Waislamu katika ardhi zao... Basi inukeni kutekeleza wajibu wenu, Mwenyezi Mungu (swt) awabariki. Simameni ili mutoe Nusrah (Msaada) yenu kwa Hizb ut Tahrir ili kusimamisha Khilafah Rashida. Sio njia pekee ya ushindi katika hali halisi ya sasa. Badala yake, ni kwa sababu ni faradhi kubwa ya daraja ya kwanza. Kwanza kabisa, yeyote asiyefanya kazi na hali ana uwezo wa kusimamisha Khilafah, na kumsimamisha Khalifa ambaye anastahiki Bayah (ahadi ya utiifu), basi dhambi yake ni kubwa kama kwamba amekufa kifo cha kabla ya Uislamu (Jahilliyah), ikidhihirisha ukali wa dhambi hilo kama alivyo sema (saw):

وَمَنْ مَاتَ وَلَيْسَ فِي عُنُقِهِ بَيْعَةٌ، مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً

**"Yeyote anayekufa na hana shingoni mwake bay'ah (ahadi ya utiifu), amekufa kifo cha kijahiliya (zama kabla ya Uislamu)."** [Muslim].

Pili, Waislamu walichukua kiapo cha Bayah kwa Khalifa, kabla ya kuanza maandalizi ya mazishi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) na kutekeleza wajibu wa mazishi yake. Yote hayo yanatokana na umuhimu wa Khalifa.

Tatu, Umar (ra) siku ya kifo chake, aliweka kikomo cha muda, cha siku tatu na si zaidi, kwa ajili ya kumchagua Khalifa miongoni mwa wale sita waliopewa bishara ya Pepo. Ikiwa hakuna makubaliano yaliyofikiwa kuhusu Khalifa, ndani ya kipindi hicho, basi mpinzani alipaswa kuuawa. Hili lilikuwa katika mkusanyiko wa Maswahaba (ra) ambao hakuna uovu wowote ulioripotiwa kuwahusu. Hivyo, ikawa ni Makubaliano ya pamoja ya Maswahaba (ra). Hata hivyo, kwetu sisi, "siku tatu nyingi sana" zimepita juu yetu! Hakika kusimamisha Khilafah ni jambo kubwa."

Na hitimisho la hitimisho lilikuwa ni kusema kwake, Mwenyezi Mungu aongoze hatua zake: "Enyi askari wa Mwenyezi Mungu: Tunatambua kwamba Malaika hawatashuka kutoka mbinguni kutuwekea Khilafah. Bali Mwenyezi Mungu (s.w.t.) atatuteremshia Malaika watusaidie tu ikiwa tutafanya kazi kwa bidii katika kusimamisha Khilafah. Ni ahadi iliyothibiti katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu.

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

**"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao"** [An-Nur 24:55]. Ni bishara njema ya izza, baada ya utawala huu dhalimu, katika hadith ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt),

***Endelea... UK 5***



ثُمَّ تَكُونُ مُلْكاً جَبْرِيَّةً فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ تَكُونَ ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ

**"...Na kisha utakuwepo utawala wa kutenza nguvu, na utakuwepo kwa muda atakao Mwenyezi Mungu uwepo kisha atauondoa anapotaka kuuondoa, kisha itakuwepo Khilafah kwa Njia ya Utume."** Kisha (saw) akanyamaza. [Imepokewa na Ahmad]. Pia tunatambua kwamba maadui wa Uislamu wanaona kusimamishwa tena Khilafah ni jambo lisilowezekana. Wanarudia kauli ya wasaidizi wao miongoni mwa wanaofanya kejeli,

غَرَّ هَؤُلَاءِ دِينُهُمْ

**"Watu hawa dini yao imewadanganya."** [Surah Al-Anfal 8:49]. Lakini kama vile msemo huo ulivyokuwa laana kwa wale waliotangulia kusema, kwani Mwenyezi Mungu ameitukuza Dini yake na akawapa ushindi watu wake, ni laana pia kwa wale wanaosema hivyo leo, kwani Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hekima, yuko pamoja na waja wake waaminifu wanaofanya kazi kwa bidii, bila ya kuachana katika nyoyo zao na viungo vyao, na kauli ya Mwenyezi Mungu (swt),

إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْراً

**"Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake."** [Surah At-Talaq 65:3]. Kila kukicha, wanazidi kukaribia Qadr "azma" hii, kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu (swt).

وَيَقُولُونَ مَتَى هُوَ قُلْ عَسَى أَنْ يَكُونَ قَرِيبًا

**"na watasema: Lini hayo? Sema: A'saa yakawa karibu!"** [Surah Al-Israa 17:51]."

Ewe Mwenyezi Mungu, uteremsha wito huu wa Amiri wetu katika nyoyo za majeshi ya Ummah wetu, na uzifanye nyoyo zao zimtamani, ili wampe nusra ya kusimamisha tena jengo la izza ya Uislamu, na turegee kama Mola wetu Mlezi alivyotutaka na kututaja kuwa ni umma bora ulioletwa kwa ajili ya watu.

إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi."** [Al-Hajj 22:70]

**Imeandikwa kwa Redio ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Muhammad Abdul Malik**

# HABARI NA MAONI
# Marekani Yazunguka Afrika Kujaribu kuziba Aibu ya Kiulimwengu ya Urasilimali

**Habari:**

Mke wa rais wa Marekani Dkt Jill Biden Mnamo siku ya Jumapili Februari 26, 2023 alitamatisha ziara yake ya siku tano katika mataifa mawili barani Afrika. Hii ilikuwa ni ziara yake ya sita barani, na ni ya kwanza huko Namibia, ya sita nchini Kenya. Ziara ya Dkt Biden inaenda sambamba na maazimio ya mkutano wa hivi karibuni wa viongozi wa Kiafrika huko Washington ambapo rais wa Marekani Joe Biden aliahidi ushirikiano zaidi na Afrika. Jill, aidha aliangazia masuala ya kuwawezesha wanawake na vijana, juhudi za kukabiliana na ukosefu wa chakula na kushajiisha maadili ya pamoja ya Kidemokrasia.

**Maoni:**

Ziara hii imekuja miezi kadhaa baada ya rais wa Marekani Joe Biden kuwaalika viongozi 49 wa nchi za Afrika jijini Washington na akaahidi kwamba “Marekani iko tayari kujali mustakabali wa Afrika”. Katika mkutano huo wa siku tatu mwezi Disemba, Biden alitangaza kwamba ataelekea barani Afrika katika msimu huu wa joto na kwamba viongozi wakuu wa utawala wake akiwemo mkewe Jill Biden, makamu rais wake Harris watafanya ziara mwaka huu kuonesha dhamira kubwa katika kushirikiana na Afrika. Kama gazeti la Washington Post, ziara ya mke wa rais ni sehemu ya azma kubwa ya kusaidia mataifa ya Afrika hasa ikizingatiwa kwamba athari ya China barani Afrika inakua ambapo wamediriki majasusi wa Kiamerika kutaja kwamba China inaangalia suala la kuipa silaha Urusi hatua ambayo waziri wa mambo ya nje wa Marekani ameitaja kwamba huenda ikawa ni “tatizo kubwa”.

Ni dhahiri kwamba Marekani inaona China kama tishio dhidi ya maslahi yake barani Afrika. Maslahi ya Marekani yanahitaji kushinikiza Afrika kuchagua, na hii kama ilivyokuwa mwanzoni pale Marekani iliposhinikiza serikali za Kiafrika kupiga kura katika baraza la Umoja wa Mataifa China ikasita kupiga kura ya kushtumu uvamizi wa Urusi nchini Ukraine. Kwa jumla diplomasia ya Marekani barani Afrika itakuwa yenye athari kubwa zaidi kama haitopangiliwa kirai ya “sisi ama wao” hasa dhidi ya China. Mapema, ndani ya utawala wa Biden Waziri wa Mambo ya nje Antony Blinken aliambia washirika wake kwamba Marekani haitowatarajia wao kuchagua baina utawala wa Washington na Beijing. Ni muhimu kuashiria kwamba tokea mwaka wa 2000 serikali ya China imekuwa ikifanya makongamano ya kibiashara baina yake na Afrika kila baada ya miaka mitatu kama mbinu ya kuimarisha mahusiano yake ya kidiplomasia na maslahi yake ya kibiashara. Kwa sasa China inatajwa kuwa ndio mshirika mkubwa wa Kibiashara wa bara la Afrika. Na taifa hili ndilo mwekezaji mkubwa katika uekezaji wa kigeni kwa Afrika ambao ni karibu mara mbili ya uekezaji wa Marekani.

Kuhusu uwezeshaji wa wanawake na vijana, ukosefu wa usalama wa chakula na Demokrasia, Dkt Jill aliweka wazi "Siku zote nimekuwa nikiamini kuwa kusaidia wanawake na vijana kote ulimwenguni ni muhimu kwa mustakabali wetu wa pamoja, pamoja na elimu, afya, na uwezeshaji katika moyo wa yote” Maoni haya yanaonyesha kejeli ya hali ya juu kwani wanajeshi wa Marekani wamekuwa wakifanya ukatili dhidi ya wanawake duniani kote kwa kibandiko cha kurejesha Demokrasia na 'vita dhidi ya ugaidi' kama ilivyo nchini Afghanistan na Somalia. Wanasiasa wa Kimagharibi akiwemo mke wa rais lazima watambue kuwa mfumo wanaouamini na kuukumbatia wa Kirasilimali na kuupigania duniani kote umesababisha ukandamizaji wa wanawake sio tu barani Afrika bali duniani kwa jumla. Wanawake na vijana wameteseka sana kutokana na kutawaliwa na hadhara ya Kimagharibi inayotokana na itikadi ya kisekula.

Kenya na Namibia bali Afrika nzima imegubikwa na viwango vikubwa vya umaskini, njaa na magonjwa. Sera mbovu za biashara zinazotetewa na Marekani na Ulaya kama vile soko huria zimesababisha maafa ya kiuchumi yanayoshuhudiwa katika bara hilo tajiri. Muhimu kutambua kwamba, sera ya Biden kwa Afrika ni mwendelezo tu wa juhudi za kibeberu kukoloni na kunyonya nchi za Kiafrika. Mipango ya Marekani, Ulaya na China inalenga kuficha aibu ya itikadi ya ubepari na si kupendelea Afrika iliyo bora zaidi. Safari hizi si nyingine bali ni mipango ya kikoloni iliyokusudiwa kuficha aibu ya Ubepari. Kwa hiyo si kweli kwamba Marekani, Ulaya na China zinaitakia mema Afrika badala yake wana ajenda ile ile ya kuisababishia madhara zaidi. Amerika na itikadi yake ya kibepari ndio chanzo pekee cha matatizo yote duniani. Wafuasi wake wanazunguka dunia nzima wakijaribu kwa siri kuficha aibu yao wenyewe, na maafa, kushindwa na mapungufu ya itikadi yao. Uislamu ndio mfumo pekee unaohitajika duniani ili kudhamini utu na hadhi ya wanawake na vijana.


**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Athari za Ushawishi wa Kijamii juu y a Waislamu Leo Wanapojitahidi Kuwa Wachaji Mungu (Muttaqeen) Wakati Wa Ramadhan

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Tsuroyya Amal Yasna**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**




Ramadhan ni mwezi ambao Mwenyezi Mungu (swt) huwawezesha Waislamu kujitafakari wenyewe kama wana wa Adam kwa kutafuta msamaha kutoka kwa Mola wao na kuweza kuwa mmoja wa Wachaji Mungu, kwani Mwenyezi Mungu (swt) anasema,

فَمَن تَابَ مِن بَعْدِ ظُلْمِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّ اللهَ يَتُوبُ عَلَيْهِ إِنَّ اللهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

**“Lakini mwenye kutubia baada ya dhulma yake, na akatengenea, basi Mwenyezi Mungu atapokea toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira na Mwenye kurehemu.”** [Al-Maida: 39]

Waislamu pia wanajua faida ambazo Mwenyezi Mungu (swt) amewezesha katika kufikia ukamilifu katika ibada zao katika mwezi huu mtukufu kama ilivyosimuliwa katika Hadith na Abu Hurairah (r.a) ambaye alisema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (saw) alisema:

إِذَا جَاءَ رَمَضَانُ فُتِّحَتْ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ وَغُلِّقَتْ أَبْوَابُ النَّارِ وَصُفِّدَتْ الشَّيَاطِينُ

**“Pindi inapokuja Ramadhan, milango ya Pepo hufunguliwa na milango na milango ya Moto hufungwa na mashetani fungwa minyororo.”** Walakini hali ya Waislamu kutafuta msamaha kutoka kwa Mola wao leo, ambapo Uislamu haupo maishani, inaweza kufupishwa kwa maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyesema;

وَاللهُ يُرِيدُ أَن يَتُوبَ عَلَيْكُمْ وَيُرِيدُ الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الشَّهَوَاتِ أَن تَمِيلُواْ مَيْلاً عَظِيمًا

**“Na Mwenyezi Mungu anataka kukurejezeni kwenye ut'iifu wake, na wanao taka kufuata matamanio wanataka mkengeuke makengeuko makubwa.”** [An-Nisa: 27].

Umbali huu ambao Waislamu wanajikuta nao kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt) na Uislamu wao wakati na baada ya Ramadhan inahusiana moja kwa moja na hali isiyo ya Kiislamu ya jamii wanazoishi ambazo zinajulikana kwa sifa ya kufuata matamanio ya mifumo iliyobuniwa na wanadamu na sio matakwa ya Muumba wetu na mfumo wa Uislamu.

Wakati wa kuisoma jamii yoyote, inaeleweka kwa usahihi sio tu kuwa na idadi ya watu wanaoishi katika eneo fulani lakini pia kuwe na mlingano wa maadili na kanuni fulani. Hizi zinazalishwa mara kwa mara na kuimarishwa katika maisha ya kila siku kwa njia ya rai jumla, vyombo vya habari, uchumi, tamaduni, sheria, siasa na kadhalika. Watu binafsi wamo ndani ya eneo hili la nguvu za kijamii ambazo bila shaka zina athari kubwa juu ya jinsi wanavyoutazama ulimwengu na wao wenyewe, na matokeo yake kutamatisha namna wanavyoishi.

Nidhamu ya kawaida tunayoiona katika jamii za Kimagharibi ni nidhamu ya kiliberali ya kisekula. Kutokana na nidhamu hii, watu binafsi na taasisi za

***Endelea... UK 8***

kijamii (serikali) ndio wanaounda fikra na hamasa za kawaida. Fikra na hamasa hizi zinazotawala zina athari ya nguvu kwa watu wote katika jamii kiasi ya kuwa aghlabu wengi wao hatimaye huanza kuzibeba fikra hizi kama zao wenyewe.

Mapungufu katika elimu na utekelezaji wa Waislamu wa dini yao sio jambo la ajali.

Mara nyingi, tunaona Waislamu wakibuni upya mifumo ya tabia za kawaida zilizosawazishwa na kurahisishwa katika jamii. Fauka ya hayo, maswala ya kibinafsi yanaoneshwa mara kwa mara, inaonesha kana kwamba Waislamu wanatarajiwa kushinda vizuizi hivi vya kimuundo kati yao na Uislamu wao kwa kitendo tu cha chaguo huru lisilo na mipaka! Kwa hivyo, wanaangazia tu kasoro kwa watu binafsi kana kwamba mifano hii iko ndani ya ombwe, pasina pia kuwa na majadiliano ya kina juu ya muktadha wao wa kijamii ni usomaji juu juu kuhusu wa tatizo, na suluhisho lolote linalotegemea hali hiyo bila shaka halitakamilika.

Wale wanaosema haya kwa kweli wamechukua mtazamo wa kibepari juu ya jamii kwani wameiangalia jamii kama yenye kujumuisha pamoja tu watu binafsi. Kutokana na hili, wamebeba mtazamo kuwa: 'Mrekebishe mtu binafsi na kisha jamii itabadilika'. Ukweli wa mambo hata hivyo ni kwamba mabadiliko au marekebisho ya mtu binafsi hupelekea marekebisho ya watu binafsi tu ambapo haina uhusiano wowote na mageuzi ya jamii. Hii ni kwa sababu jamii sio tu ni mkusanyiko wa watu binafsi bali ni watu ambao wana uhusiano wa kudumu ambao huwaunganisha pamoja. Kwa hivyo, kusahihisha mahusiano ndio hupelekea usahihishaji wa jamii. Mahusiano haya ni mkusanyiko wa fikra na hisia ambazo zinalindwa (na kudumishwa) na Nidhamu (serikali). Mwenyezi (swt) ameteremsha:

إِنَّ اللَّهَ لاَ يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّى يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ

**"Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo naf- sini mwao."** [Ar-Ra'd 13:11].

Maana ya aya hii sio, kama wengine wanavyoitumia, kuwa mabadiliko hayo hayatatokea katika jamii au kwa watu hadi watu wote wabadilike. Bali, ni kwamba mabadiliko hayatatokea hadi jamii ibadilishe yaliyomo ndani yake ambayo yanajumuisha watu binafsi lakini pia hujumuisha fikra zao, hisia zao na nidhamu yao ndani ya jamii. Ndio sababu ni muhimu kwetu, ambao tunataka kubadilisha jamii, kuifafanua kwa usahihi.

Kwa hivyo, ikiwa Nidhamu ni ya Kiislamu inayolinda na kuhifadhi fikra na hisia za Kiislamu, itawakilisha jamii ya Kiislamu hata kama watu wake wengi hawakuwa Waislamu. Ikiwa, hata hivyo, nidhamu ni ya kikafiri inayolinda hisia na fikra zisizokuwa za Kiislamu, basi jamii hiyo itakuwa isiyokuwa ya Kiislamu na hata kama wengi wa watu wake walikuwa Waislamu!! Kwa hivyo, rangi muhimu zaidi ambayo hutofautisha jamii ni Nidhamu.

Kwa hivyo kutambua umuhimu ambao mifumo ya wanadamu inao juu ya Waislamu inapaswa kusababisha kwa Waislamu kutambua haja ya sio tu kujitahidi kibinafsi kutafuta radhi ya Mola wao ndani ya Ramadhan hii kwa kusoma maana ya ayat za Qur'an tukufu, kusoma juu ya maisha ya Mtume (saw) na masahaba zake (ra): jinsi walivyoishi maisha yao, jinsi walivyojitoa muhanga maisha yao na viungo vyao kuufanya ulimwengu wa Mwenyezi Mungu (swt) kuwa juu lakini pia kusoma juu ya sheria za mwingiliano katika Uislamu iwe katika biashara, fedha, kilimo au mengine. Hebu natutazame kile ambacho Uislamu unasema juu ya uhusiano kati ya wanaume na wanawake, familia na watoto. Uislamu ni mfumo kamili wa maisha na katika mwezi huu uliobarikiwa, hebu natuweke nia ya dhati kugusia sehemu zingine za Uislamu ambazo hatuna maarifa nazo tunapofanya kazi ya kuleta mabadiliko ya kijamii kutoka kwa nidhamu zilizotungwa na wanadamu hadi kwa nidhamu za Uislamu.

# بسم الله الرحمن الرحيم

# إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

**“Wewe tu Tunakuabudu, na Wewe tu Tunakuomba Msaada”** [Al-Fatiha: 5]

Kila siku, katika kila swala, ya faradhi au nafila, Waislamu wanasoma kauli ya Mwenyezi Mungu (swt), aya katika Surat Al-Fatiha:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

**“Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada”**

Hivyo, Waislamu wanakiri na kutangaza kujisalimisha kwao kwa Mwenyezi Mungu (swt), na watakuwa na Tawhid, watamtii Yeye, watamuabudu Yeye Peke Yake na kutaka msaada kutoka Kwake (swt) katika kuabudu kwao, utiifu wao katika mambo yao yote. Imeelezwa kwenye tafsiri ya Ibn Kathir: “Hatumuabudu yeyote isipokuwa Wewe, na hatumtegemei yeyote isipokuwa Wewe, na huu ndio ukamilifu wa utiifu.” Dini inaegemea juu ya maana hizi mbili, na baadhi ya waliotangulia wamesema: al-Fatiha ndio siri ya Qur’an, na siri yake ni tamko hili:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

**“Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada”** [Al-Fatiha: 5].

Kipande cha kwanza kinakataa kumshirikisha Mwenyezi Mungu (swt), na cha pili kinakataa uweza na nguvu, na kinayapeleka mambo kwa Mwenyezi Mungu (swt). Maana hii inapatikana kwenye zaidi ya aya moja ya Qur’an, Mwenyezi Mungu (swt) anasema:

فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ

**“Basi Muabudu Yeye na umtegemee Yeye. Na Mola wako Mlezi haghafiliki na yale mnayoyatenda”** [Hud: 123]

قُلْ هُوَ الرَّحْمَنُ آمَنَّا بِهِ وَعَلَيْهِ تَوَكَّلْنَا

**“Sema, Yeye ni mwingi wa Rehema; tunamuamini Yeye, na juu Yake tunategemea”** [Al-Mulk: 29]

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلاً

**“Mola Mlezi wa mashariki na magharibi, hapana mungu isipokuwa Yeye, basi mfanye awe mtegemewa wako.”** [Al-Muzzammil: 9]. Pamoja na aya hii tukufu:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

**“Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada”** [Al-Fatiha: 5].

Ni sharti kwa ibada ili ikubaliwe na Mwenyezi Mungu (swt) ni kuwa ifanywe kwa ajili Yake tu. Mwenyezi Mungu (swt) anasema:

قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ مُخْلِصاً لَّهُ الدِّينَ

**“Sema: Hakika mimi nimeamrishwa nimuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia Dini Yeye tu.”** [Az-Zummar: 11].

Na Mwenyezi Mungu (swt) anasema:

***Endelea... UK 10***

وَمَا أُمِرُواْ إِلَّا لِيَعْبُدُواْ اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُواْ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُواْ الزَّكَاةَ وَذَلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ

**“Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na washike Swala, na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini Madhubuti.”** [Al-Bayyina: 5].

Unyenyekevu ni kumchagua Mwenyezi Mungu (swt) kwa nia ya kuabudu na kutegemea malipo kutoka Kwake Pekee.

Kutoka kwa Abu Huraira (ra), kuwa Mtume (saw) amesema:

قَالَ اللَّهُ تَبَارَكَ وَتَعَالَى: أَنَا أَغْنَى الشُّرَكَاءِ عَنِ الشِّرْكِ، مَنْ عَمِلَ عَمَلاً أَشْرَكَ فِيهِ مَعِي غَيْرِي تَرَكْتُهُ وَشِرْكَهُ

**“Mwenyezi Mungu aliyetukuka amesema: Mimi nimejitosheleza kiasi kuwa sihitaji mshirika. Atakayefanya amali kwa ajili ya mwengine pamoja nami, nitamuachia na washirika wake.”** [Ameipokea Muslim].

Pia inatakiwa ibada iwe kwa namna na njia ambayo Mwenyezi Mungu (swt) ametuagiza na kutufundisha Mtume Wake (saw). Kutekeleza ibada kunahitaji elimu juu ya ibada na elimu ya hukmu zake na namna ya kuzitekeleza kabla ya utekelezaji wake.

Kuwa mja wa Mwenyezi Mungu (swt) kuna maanisha kutekeleza maamrisho Yake na kujifunga na hukmu Zake katika kila kitu alichokiamrisha na alichokikataza. Ibada katika maana yake ya jumla haijajifunga katika kutekeleza matendo ya kibinafsi tu yanayoambatana na mahusiano yake na Mola Wake, kama swala, funga, zaka na Hajj, bali imekusanya matendo yanayohusisha mahusiano ya mtu na nafsi yake mwenyewe kama vyakula na nguo, na mahusiano yake na watu wengine kama miamala, ujenzi wa ardhi na urithi ndani yake na kufanya kazi kutekeleza sheria Zake (swt) katika ardhi na kubeba ujumbe wa Uislamu na ulinganizi wake ulimwenguni.

Kuwa mja wa Mwenyezi Mungu (swt) maana yake ni kutaka msaada Wake kutenda matendo ya utiifu na ibada, na kutaka msaada Wake katika kujiweka mbali na makatazo Yake pamoja na kuushinda ushawishi wa Shetani na minong’ono ya nafsi inayoamrisha uovu.

Imepokewa na Mu’adh bin Jabal (ra) kuwa Mtume (saw) ameniambia,

أُوصِيكَ يَا مُعَاذُ، لَا تَدَعَنَّ فِي دُبُرِ كُلِّ صَلَاةٍ أَنْ تَقُولَ: اللَّهُمَّ أَعِنِّي عَلَى ذِكْرِكَ وَشُكْرِكَ وَحُسْنِ عِبَادَتِكَ **“Nakuusia ewe Mu’adh, Usiwache kusema katika kila mwisho wa swala: ‘Ewe Mwenyezi Mungu, nisaidie katika kukukumbuka, na kukushukuru, na kukuabudu kwa vizuri.”** [Imepokewa na Abu Dawud na wengineo]

Hii ina maana kuwa tunahitaji msaada Wake katika mambo yetu yote ya maisha na kuwa tunarejea Kwake na kumtaka msaada Wake katika madhara yote yanayotupata na katika madhara na mazito yanayotupata katika kulingania Uislamu na katika juhudi zetu katika kusimamisha dini yake juu ya ardhi, na tukilenga juu ya kauli ya Mwenyezi Mungu (swt):

وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْراً

**“Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake.”** [At-Talaq: 3].

Ina maana kuwa hatujisalimishi kwa madhalimu na maadui wa Dini, na hatuwarudii na kutaka msaada kwao, kwani Mwenyezi Mungu (swt) yuko pamoja nasi, na nguvu zao na ufalme wao utaondoka bila kujali muda utakaochukua. Mwenyezi Mungu (swt) bila shaka atatusaidia, na yeyote anayemtegemea Mwenyezi Mungu (swt) hatojuta, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

Mwezi wa Ramadhan ni fursa kubwa kuifanya upya ahadi ya Mwenyezi Mungu (swt), na kukubali kutii kwetu kujisalimisha Kwake (swt), na hukumu Zake; na kutupatia utiifu na kuabudu, kufanya kazi ya kubadilisha hali hii fisidifu, kutaka msaada wa Mwenyezi Mungu (swt), kumuamini Yeye, na kuamini ushindi Wake, basi na tusonge mbele katika njia hii na tusimame kidete na kufanya kazi kwa bidii.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Bara’ah Manasrah**

 Pepe: info@uqab.or.ke

# JIBU LA SWALI

# Zaka juu ya Bidhaa za Biashara




**Swali:**

Namaanisha, zaka ya bidhaa za biashara ni thamani ya bidhaa inayotolewa kwa ajili ya kuuzwa, thamani ya kuiuza kutoka kwa mlipaji zaka kwa wateja wake, sio thamani ambayo mlipaji zaka anainunulia kwayo!

Ikiwa nilinunua simu za rununu 10,000 na kuziuza kwa 15,000. Zaka itakuwa kutokana na 15,000.

Je, hii ni sahihi?!

**Jibu:**

**Katika Kitabu ya Al-Amwaal:** [Zaka juu ya Bidhaa za Biashara

Bidhaa za biashara ni kila kitu isipokuwa sarafu inayotumika kufanya biashara, kununua na kuuza, kwa ajili ya faida k.m. vyakula, nguo, samani, bidhaa za viwandani, wanyama, madini, ardhi, majengo na bidhaa nyinginezo zinazonunuliwa na kuuzwa.

Zaka inawajibika kwa bidhaa zinazochukuliwa kwa ajili ya biashara kwa makubaliano ya wanachuoni wa awali na wa baadaye. Kutoka kwa Samura b. Jundub ambaye alisema:

أَمَّا بَعْدُ، فَإِنَّ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ كَانَ يَأْمُرُنَا أَنْ نُخْرِجَ الصَّدَقَةَ مِنَ الَّذِي نُعِدُّ لِلْبَيْعِ

**"Ama baada ya swala na salamu! Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akituamrisha kutoa Zaka kwa vile tulivyoovitayarisha kwa ajili ya kuviuza"** (Imepokewa na Abu Dawud). Imepokewa kutoka kwa Abu Dharr kutoka kwa Mtume ambaye amesema: وَفِي الْبَزِّ صَدَقَتُهُ **"Kuna Zaka katika Bazz."** Imesimuliwa na Al-Daraqutni na Al-Bayhaqi. Al-Bazz ni nguo na vitambaa vya kusuka zinazotumika kwa biashara. Abu 'Amra b. Hamas amepokea kutoka kwa babake ambaye alisema: "'Umar ibn Al-Khattab alipita na akasema: 'Ewe Hamas, toa Zaka katika mali yako'. Nikasema: 'Sina mali yoyote isipokuwa Ji'b (podo za mishale) na ngozi'. Akasema: 'Zikadirie, kisha toa Zaka zao.'" AbdurRahman b. Abdul-Qari alisema: "Niliteuliwa juu ya Bait ul-Mal katika zama za 'Umar ibn Al-Khattab. Zawadi zilipotolewa, mali ya wafanyibiashara ilikusanywa na kuhesabiwa, kwa kile kilichopo au kisichokuwepo." Kisha Zaka ikachukuliwa kutoka katika mali ya sasa kwa ile iliyokuwepo na isiyokuwepo." Kutoka kwa ibn 'Umar ambaye amesema: "Kuna Zaka ya Raqiiq (watumwa) na suti za Bazz ambazo zinakusudiwa kufanyiwa biashara." Faradhi ya Zaka katika biashara imesimuliwa kutoka kwa Umar na mwanawe, ibn Abbas, mafaqihi saba, Al-Hassan, Jabir, Tawus, Al-Nakhai, Ath-Thawri, Al-Awzai, Ashl-Shafii, Ahmad, Abu Ubaid, watu wa rai (As'hab ar-Rai), Abu Hanifah na wengineo.

***Endelea... UK 12***


Pepe: info@uqab.or.ke

Zaka ya bidhaa za biashara ni wajibu inapofikia thamani ya Nisab ya dhahabu na fedha, na kuzungukiwa na mwaka.

I**kiwa mfanyibiashara ataanza biashara yake kwa mali iliyo chini ya Nisab kisha ikafika Nisab mwishoni mwa mwaka, hakuna Zaka juu yake kwa sababu mwaka haujapita juu yake. Zaka italazimika katika Nisab yake baada ya kupita mwaka mzima juu yake.**

**Iwapo mfanyibiashara ataanza biashara yake na mali iliyo juu ya Nisab kiasi kwamba anaanza biashara yake kwa Dinari 1,000 kisha biashara yake ikakua na kupata faida ifikapo mwisho wa mwaka na thamani yake ikawa Dinari 3,000, ni wajibu kwake kulipa Zaka juu ya 3,000 Dinari sio Dinari 1,000 alizoanza nazo. Hii ni kwa sababu faida yake inafuatana nayo yaani asili, na kipindi cha mwaka mmoja wa faida inayozalishwa ni sawa na kipindi cha mwaka mmoja wa asili.** Hii ni kama watoto wa mbuzi (Sikhal) na wa kondoo (Baham), wanaohesabiwa pamoja nao, kwa sababu muda wao wa mwaka mmoja (Hawl) ni wa mama zao. Sawia na hii ni faida kwenye mali hivyo wakati wake (Hawl) ni kipindi cha mwaka mmoja wa asili ambayo faida ilipatikana. **Pindi mwaka unapokwisha mfanyibiashara hukadiria bidhaa ya biashara** yake iwe Zaka ni wajibu juu yake kwa sababu ya aina ya bidhaa yenyewe kama ngamia, ng'ombe na kondoo, au la, kama nguo, bidhaa za viwandani, ardhi na majengo. **Anazikadiria zote kwa pamoja kwa vipimo vya dhahabu au fedha. Kisha anatoa zaka ya robo ya ushuri ikiwa itafikia thamani ya Nisab ya dhahabu au fedha, akitoa Zaka ya faradhi kwa sarafu inayotumika.**

Inaruhusiwa kwake kutoa Zaka yake kwa bidhaa yenyewe ikiwa hilo ni rahisi kwake, k.m. pale anapofanya biashara ya kondoo/mbuzi, ng'ombe au nguo na thamani ya Zakat anayolazimika kukadiriwa kuwa ni kondoo, ng'ombe au nguo, anaweza kutoa Zaka yake kwa fedha au kutoa kwa kondoo, ng'ombe au nguo yaani anaweza kutoa chochote anachotaka.

Zaka ya bidhaa za biashara, ambayo mali yake inatozwa kama ngamia, ng'ombe na kondoo / mbuzi, inatolewa kama Zaka ya biashara, sio Zaka ya mifugo. Hii ni kwa sababu biashara ndiyo inayokusudiwa katika umiliki wao, sio umiliki tu...]. **MWISHO.**

Kwa hivyo biashara inakadiriwa mwanzoni, na ikiwa imefikia nisab au zaidi, hii inahesabiwa kuwa ni mwanzo wa mwaka na mwisho wa mwaka inafanywa tena, basi zaka yake hutolewa kulingana na makadirio wakati zaka inapostahiki, na kama ilivyotajwa hapo juu, faida inajumuishwa wakati wa kuhesabu thamani ya biashara hata kama mwaka mmoja haujapita, kwa sababu faida inahusiana na mtaji.

**Yaani, makadirio ya biashara ni mwanzoni mwa nisab, kisha baada ya mwisho wa mwaka kutoka mwanzo wa nisab, yaani, wakati zaka inapostahiki.**

Natumai hii inatosheleza, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Zaidi na Mwingi wa hekima.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**28 Sha'aban 1444 H**
**Sawia na 20/03/2023 M**

***Endelea... UK 8***